



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



## HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. JA.75/345/01/33

24/04/2023

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kufuatia Serikali kutoa idhini ya Utekelezaji wa Ikama na Bajeti kwa Ajira Mpya katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, kwa Kibali chenye Kumb. Na. FA.97/228/01 "TEMP"/06 cha Tarehe 06 Aprili, 2023, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inatangaza nafasi ya Ajira kwa Kada ya Madereva kwa Watanzania wenye sifa kama ilivyoainishwa hapa chini:-

### DEREVA DARAJA LA II – NAFASI MBILI (2)

#### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Cheti cha Kidato cha Nne (Form Four) na Leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua Mwaka Mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi (VETA) au Chuo kingine. Waombaji wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

#### 1.2 KAZI/MAJUKUMU YA KUFANYA

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iii. Kufanya Matengenezo madogomadogo ya gari
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- vi. Kufanya Usafi wa gari na
- vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

#### 1.3 MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara wa Serikali TGS.B.1

**NB: MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI:-**

- i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania ambao hawazidi umri zaidi ya miaka 45 na hawapungui umri wa miaka 18,
- ii. Waombaji wote lazima waambatanishe wasifu binafsi (CV) wenye mawasiliano ya uhakika, anuani, barua pepe na namba za simu.
- iii. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya **TANGAZO LA KAZI**.
- iv. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo
  - a) Cheti cha Msingi cha Uendeshaji Magari kulingana na sifa za nafasi husika.
  - b) Cheti cha mtihani wa kidao cha nne au sita,
  - c) Cheti cha kuzaliwa.
  - d) Nakala ya Kitambulisho cha Uraia (NIDA)
- v. Hati ya matokeo ya kidato cha nne (Result slip) haitafanyiwa kazi.
- vi. "Transcript" ambayo haikuambatanishwa na cheti haitafanyiwa kazi.
- vii. Kuwasilisha vyeti vya kughushi na maelezo mengine itasababisha kuchukuliwa hatua za kisheria.
- viii. Watumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
- ix. Waombaji ambao walistaafu kazi kwa sababu yoyote ile hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
- x. Waombaji waonyeshe wadhamini wawili na mawasiliano yao, anuani na namba za simu.
- xi. Waombaji wenye vyeti ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya ufundi la Taifa (NACTE) na Tume ya Vyujo Vikuu (TCU).
- xii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au kiingereza.
- xiii. Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri – [www.kinondonimc.go.tz](http://www.kinondonimc.go.tz)
- xiv. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **07 Mei, 2023** saa tisa na nusu (**9:30**) Alasiri.
- xv. Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Manispaa.
- xvi. Maombi yatakayolewa kwa mkono hayatapokelewa na hayatafanyiwa kazi
- xvii. Maombi yote yatumwe kwa Anuani ainishwa hapa chini na si vinginevyo :-

**Mkurugenzi wa Manispaa,  
Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni,  
S.L.P. 31902,  
DAR ES SALAAM.**



*Hanifa S. Hamza*

**MKURUGENZI WA MANISPAA**